



## BENKI KUU YA TANZANIA

### TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

#### **MADAI KUWA “ASILIMIA 45 YA MABOSI WA BENKI KUU WAKABILIWA NA KESI ZA UFISADI”**

Tarehe 22 Septemba 2009 gazeti la NIPASHE lilichapisha habari iliyopewa uzito mkubwa katika ukurasa wa mbele kuonyesha kwamba “asilimia 45 ya mabosi wa Benki Kuu wakabiliwa na kesi za ufisadi”.

Mwandishi wa habari hiyo alieleza kwamba kufuatia kufikishwa mahakamani wiki iliyopita wakurugenzi wanne wa Benki Kuu ya Tanzania kwa tuhuma za kuhujumu uchumi, idadi ya wakurugenzi wa Benki Kuu ya Tanzania wanaokabiliwa na kesi wanakaribia kufikia nusu ya wakurugenzi wote wa taasisi hii.

Kwa mujibu wa gazeti hilo, Benki Kuu ina kurugenzi kumi na moja (11) kulingana na muundo mpya ambapo hadi wiki iliyopita wakurugenzi watano wamefikishwa kortini kwa tuhuma tofauti za wizi, kuisababishia serikali hasara au kuhujumu uchumi.

Uongozi wa Benki Kuu ya Tanzania umesikitishwa na taarifa hiyo na unapenda kuwaarifu wananchi na wadau wake wote kwamba taarifa ya gazeti hilo la NIPASHE siyo sahihi na ni ya kupotosha.

Ukweli ni kwamba wakati kesi zinazohusu tuhuma za kusababishia serikali hasara kupitia shughuli za Akaunti ya Madeni ya Nje (EPA) zinaanza mwaka 2008, Benki Kuu ya Tanzania ilikuwa na jumla ya Kurugenzi kumi na saba (17) na siyo kumi na moja (11) kama gazeti lilitoyodai. Vile vile, katika muundo wa Benki Kuu uliopo ambao umefanyiwa marekebisho kadhaa kuanzia mwezi Agosti 2009, idadi ya kurugenzi imebakia kumi na saba na si kumi na moja. Idadi hiyo haijumuishi Mameneja (au Manaibu Wakurugenzi kama walivyokuwa wanafahamika kabla ya mabadiliko ya muundo).

Tunapenda ieleweke pia kuwa siyo kweli kwamba watuhumiwa wote waliofikishwa mahakamani walikuwa katika nyadhifa za uongozi, yaani wakurugenzi kama mwandishi wa habari anavyotaka umma uamini.

Kwa mujibu wa kumbukumbu sahihi zilizopo, ni watuhumiwa wawili tu ambao walikuwa katika ngazi za ukurugenzi wakati wanafikishwa mahakamani.

Watuhumiwa wengine wamefikishwa mahakamani wakiwa wamestaafu au kuachishwa kazi na wengine kati ya hao hawajawahi kushika nafasi za uongozi tofauti na taarifa ya gazeti inavyoonyesha. Kwa idadi hiyo ya Wakurugenzi na kurugenzi zilizopo sasa baada ya muundo mpya na hata katika muundo wa zamani, uwiano wa idadi hiyo ya wakurugenzi waliofikishwa mahakamani ni asilimia 11.76 (11.76%) ya wakurugenzi wote waliopo Benki Kuu. Kwa msingi huu siyo kweli na ni upotoshaji mkubwa kudai kwamba asilimia 45 ya wakurugenzi wa Benki Kuu ya Tanzania wanakabiliwa na kesi mahakamani.

Kwa ujumla taarifa ya “tathmini” ya gazeti la NIPASHE la tarehe 22 Septemba 2009 imetoa taarifa nyingi zisizo sahihi na ambazo zinajikanganya na kwa ujumla imeshindwa kuzingatia kwamba kilichopo mahakamani ni tuhuma tu na zitahitaji kuthibitishwa. Tunaomba wananchi na wadau wetu kuelewa kuwa Benki Kuu ya Tanzania ni taasisi nyeti ya serikali yenye dhima kubwa katika masuala ya kusimamia uchumi, na gazeti la NIPASHE linakiri waziwazi.

Kwa hiyo ni vema waandishi wa habari wakatoa picha sahihi ya mambo yanayoendelea kwa kuzingatia maadili ya taaluma yao na kuepuka taarifa za upotoshaji. Ni muhimu vile vile waandishi wa habari kama wadau katika maendeleo ya nchi watimize wajibu wao kwa kuandika, pamoja na matukio mbalimbali, taarifa muhimu na sahihi kuhusu jitihada kubwa ambazo Benki Kuu ya Tanzania inafanya katika kuboresha utendaji na mchango wake katika kukuza uchumi wa nchi yetu.

(Imesainiwa)

**BENKI KUU YA TANZANIA**

23 Septemba 2009